

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA
SHULE YA SEKONDARI DODOMEZI,

S.L.P 142,
KILWA-MASOKO
14/12/2019.
BARUA PEPE: dodomezi.school@yahoo.com
MOBILE NO: 0787070743/0787936265

Kumb Na. DSS/REG.NO./2654/14

Jina la mwanafunzi.....

.....

S.L.P.....

KILWA MASOKO.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI DODOMEZI
WILAYA YA KILWA MKOA LINDI MWAKA 2021.

Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha 1 katika shule hii mwaka 2020. Shule ya sekondari **DODOMEZI** ipo umbali wa km 30 kutoka makao makuu ya wilaya. Muhula wa kuanza wa masomo utanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 17/01/2020 ndani ya siku saba.

Masomo anayotakiwa kusoma kidato cha kwanza ni tisa ya msingi ambayo ni:

- | | |
|----------------------------------|---|
| i. Uraia (civics) | vi. Kemia (chemistry) |
| ii. Historia (history) | vii. Biolojia (biology) |
| iii. Jiografia (geography) | viii. Hisabati (basic mathematics) |
| iv. Kiswahili | ix. Fizikia (physics) |
| v. Kiingereza (english language) | x. Elimu ya dini ya kiislamu – Somo hili ni la hiari. |

Mambo muhimu ya kuzingatia

1. SARE ZA SHULE

A. Sare za darasani

Wavulana

- i. Suruali (2) za rangi ya kahawia
- ii. Mashati meupe mawili
- iii. Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili
- iv. Soksi ndefu nyeupe jozi mbili
- v. Mkanda mweusi
- vi. T-shirt ya shule inapatikana shuleni kwa shilingi 15,000/=
- vii. Tai na nembo ya shule ni shilingi 5000/= vinapatikana shuleni

NB:- Suruali iwe pana kuanzia inchi saba na kuendelea.

Wasichana

- i. Sketi (2) za kahawia, Mshono ni **SKETI YA RINDA BOKSI.**
- ii. Mashati meupe mawili
- iii. Wasichana wanaruhusiwa kuvaa **HIJABU**

SIFA ZA HIJABU

- Nusu kanzu mbili nyeupe yenye mikono mirefu na urefu kwenda chini ukaribie magoti isibane mwili na kitambaa kisionyeshe maumbo ya ndani.
 - Sketi mbili ndefu zinazokaribia kisigino
 - Kilemba cha kichwani (HIJABU) nyeupe ya kawaida isiwe na mapambo na iwe ya duara inayokaribia vifundo vya mikono.
- iv. Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili.
- v. Soksi ndefu nyeupe jozi mbili.
- vi. T-shirt ya shule inapatikana shuleni kwa shilingi 15,000/=
- vii. Tai na nembo ya shule ni shilingi 5000/= vinapatikana shuleni.
- Angalizo** mwanafunzi atakaeshona sare ya shule tofauti na maelekezo hatopokelewa shuleni

B. Sare ya michezo

Wavulana

- Fulana 2 na bukta 2 za njano
- Viatu vya Raba jozi moja

Wasichana

- Fulana 2 na bukta 2 za bluu
- Track Suti jozi moja.
- Viatu vya Raba jozi moja

2. Picha nne (4) za passport size ukiwa umevaa shati au Hijabu ya shule

3. VIFAA VYA KUJIFUNZIA

- Ream moja kwa ajili ya mitihani mbalimbali
- Faili mbili kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zake la Plastic (**Spring file**)
- Daftari 10 aina ya kaunta kalamu na mkebe wa hesabu na daftari moja ya mazoezi kwa kila somo liloorodheshwa hapo juu.

NB: Vifaa hivyo pia vinapatikana shuleni hivyo unaweza kuja na fedha kwa ajili ya kununua vifaa hivyo

Mchanganuo wa bei ya vifaa hivyo:-

| S/N | AINA YA KIFAA | BEI YA KILA KIMOJA |
|-----|----------------|--------------------|
| 1. | RULA | 500/= |
| 2. | KAUNTA QUIRE 2 | 2,500/= |
| 3. | PENI | 200/= |
| 4. | PENSELI | 100/= |
| 5. | UFUTIO | 300/= |
| 6. | DAFTARI MSOMI | 500/= |
| 7. | MKEBE | 2,500/= |
| 8. | RIMU | 12,000/= |
| 9. | FOUR FIGURE | 3,000/= |
| 10. | SOKSI | 1,500/= |
| 11. | MAJALADIO | 300/= |
| 12. | FILE | 1000/= |

4. VIFAA VYA USAFI.

a) *Ufagio wa wima mmoja au fedha (Tsh 2,000/=)*

5. Mchango wa maji 1,000/= kwa mwezi

6. - Mchango wa chakula kwa wanafunzi wa kutwa Tsh. 15,000/= kwa mwezi, kwa siku 700 AU Mahitaji yafuatayo:-

- a) Unga kilo 5.
- b) Maharage kilo 2.5
- c) Mpishi (Tsh 3,000/=)

- Mchango wa chakula kwa wanafunzi watakaoshi hosteli Tsh. 60,000/= kwa mwezi, kwa siku 2,000/= AU
Mahitaji yafuatayo:-

- a) Unga kilo 10.
- b) Mchele kilo 5.
- c) Maharage kilo 5
- d) Mafuta ya kupikia lita 2.
- e) Sukari kilo 2.
- f) Chumvi pkt 1
- g) Vituguu kg 1 na nusu.(Tsh.3,000/=)
- h) Mbogamboga Tsh 7,500/=
- i) Mpishi 5,000/=

6. Kwa wanafunzi watakaoshi hosteli watatakiwa kufika shuleni pamoja na wazazi/walezi wao siku ya tarehe 05/01/2019 saa 1 asubuhi wakiwa na vifaa vifuatavyo:-

- Godoro la futi tatu (3)
- Ndoo ndogo ya maji
- Tochi/taa ya sola kwa ajili ya dharura
- Shuka mbili za rangi ya buluu na pinki
- Vifaa vya usafi (mafuta, sabuni, kitana)
- Kikombe cha uji, kijiko, bakuli na sahani ya chakula

Mambo Mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na wanafunzi.

- a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na **Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali** baada ya vipimo. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo, na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

ANGALIZO:

1. **Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu kama ilivyoelekezwa na si vinginevyo.**
2. **Mwanafunzi wa kike anatakiwa kukaa Hosteli.**

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI DODOMEZI

.....
MOSI H. KARANJE
MKUU WA SHULE

3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya RAIS - TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni-preparations (kwa wabweni).
- d) Kuwahi shule kuanzia saa 12:45 asubuhi na katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kiakamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira yote.
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, na
- i) Kutunza mali za umma.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE.

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyo kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli, na kadhalika.
- e) Kupigana au kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g) Kudharau bendera ya Taifa
- h) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
- i) Kuoja au kuolewa
- j) Kutoa mimba
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu wa jamii inayomzunguka.
- l) Kukataa adhabu ya mwalimu kwa makusudi.
- m) Kuwa na simu ya mkononi.

UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI

Mimi _____ ninakubali mtoto wangu _____ asome katika shule ya sekondari Dodomezi nitahakikisha wakati wote mwanangu atapokuwa anasoma hapa shuleni:-

A. Atakuwa hana ruhusa ya kwenda katika majumba ya wageni maeneo ya ulevi. Mataarabu n.k.

B. Ninaahidi kumpa vifaa vyote vinavyohitajika na ninathibitisha atakuwa na mahali pa kulala muda wote mpaka amalize masomo yake.

C. Ninaelewa kuwa nafasi hii ya mtoto wangu kuingia Elimu ya sekondari siyo haki yake ila ni bahati aliyotunukiwa na Taifa kwa jinsi hiyo ninaahidi nitahakikisha anafuata sheria za shule na pale atakaposhindwa hatua ipasayo ichukuliwe dhidi yake.

D. Ninaahidi kumleta shuleni wakati uliopangwa bila kuchelewa ili nafasi yake isije ikachukuliwa na wengine.

E. Mwanangu akiwa shuleni alelewe katika dini ya _____

F. Anuani _____ yangu

G. Sahihi yangu mimi mzazi/mlezi _____

Tarehe _____

H. Sahihi ya mtoto _____

Tarehe _____

I. Ndugu wengine wa karibu wanaoweza kufuatilia matatizo/maendeleo ya mtoto huyu ni:-

| Nº | JINA | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU |
|----|------|----------|---------------|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE AND TECHNOLOGY
KILWA DISTRICT COUNCIL
DODOMEZI SECONDARY SCHOOL**

THE HEADMASTER OFFICE,
P.OBOX 142,
KILWA MASOKO.
Date:

TO THE MEDICAL OFFICER

.....
.....

SPEEECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Name of student.....form.....term.....year.....

Dear Doctor,

I shall grateful if you examine the above named student and send us a report regarding his/her health condition for his/her suitability in undertaking studies.

1. X-Ray (), 2. Urine (), 3. Stool (), 4. V.D (), 5. Tuberculosis (), 6. Physical fitness (), 7. Pregnancy ().

A: PRELIMINARY INFORMATION BY THE STUDENTS BEFORE THE DOCTOR

| S/N. | DISEASE | YES | NO | S/N. | DISEASE | YES | NO |
|------|----------------------------|-----|----|------|-------------------------------|-----|----|
| 1. | Tuberculosis | | | 11. | Epilepsy | | |
| 2. | Pneumonia | | | 12. | Ear, nose and throat troubles | | |
| 3. | Asthma | | | 13. | Skin disorder disease | | |
| 4. | Heart trouble | | | 14. | Anemia | | |
| 5. | Recurrent indigestion | | | 15. | Operations | | |
| 6. | Jaundice | | | 16. | Serious accident | | |
| 7. | Dysentery | | | 17. | Stomach trouble | | |
| 8. | Kidney and Urinary trouble | | | 18. | Eye disorder | | |
| 9. | Nervous breakdown | | | | | | |
| 10. | Diabetes | | | | | | |

B: VITAL STASTICS

Age Height beat Blood pressure Vision ectWeight

3. OFFICIAL MEDICAL EXAMINATION REPORT

I have examined Mr/Miss and consider that he/she is fit/unfit to be admitted to Dodomezi Secondary School.

Name:.....

Signature:.....

Title.....

Qualification.....

Official stamp:

Date.....

.....

**SHULE YA SEKONDARI DODOMEZI
TAARIFA MAALUMU KUHUSU MWANAFUNZI MPYA**

SEHEMU A

Jina kamili (Kwa herufi kubwa)

Tarehe ya kuzaliwa

Kabila Dini

Anuani ya nyumbani

Kata Tarafa Wilaya

SEHEMU B:

Jina la Baba/Mlezi anaishi/amefariki

Kazi ya Baba/mlezi Namba ya simu

Jina la Mama/Mlezi anaishi/amefariki

Kazi ya Mama/mlezi Namba ya simu

JINA NA UMRI WA (KAKA NA DADA)

| JINA LA NDUGU | KIWANGO CHA ELIMU | ANUANI YAKE |
|----------------------|--------------------------|--------------------|
| | | |
| | | |
| | | |

SEHEMU C: FANI UNAZOPENDELEA

| JINA LA MCHEZO AU NGOMA | SHULE AU MAHALI | TOKA MWAKA | MPAKA MWAKA |
|--------------------------------|------------------------|-------------------|--------------------|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**SEHEMU D: KAZI YOYOTE YA UONGOZI ULIYOWAHI KUFANYA MFANO KIONGOZI
WA MICHEZO, NGOMA N.K**

| MADARAKA AU KAZI | SHULE AU MAHALI | TOKA MWAKA | MPAKA MWAKA |
|-------------------------|------------------------|-------------------|--------------------|
| | | | |
| | | | |

Naahidi kuwa nitakuwa mwanafunzi mzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.

Sahihi ya mwanafunzi

Sahihi ya mzazi / mlezi

Tarehe